



# Kutumia madumu yenye matundu kuongeza ubora wa samaki

## Kutunza ubora wa samaki

Samaki ni chakula chenye virutubisho vingi vinavyoweza kutunza afya ya akili, mwili na hata ngozi. Hata hivyo, samaki wabichi wanaharibika haraka. Kutunza ubora wake kuna maana kwamba wavuvi, wachakataji na wafanyabiashara wanapaswa kushughulika na samaki kwa umakini mkubwa kwa kutumia vifaa sahihi wakati wa kuvua na kuwasafirisha. Samaki wenye ubora huvutia bei ya juu, wakati wale wenye ubora duni husababisha hasara.



©FAO/Ansen Ward

## Vitu vinavyopunguza ubora wa samaki

Vitu vinavyopunguza ubora wa samaki ni pamoja na kiwango cha juu cha unyevunyevu, joto lisilo na uwiano mzuri, ushughulikaji wa samaki usiozingatia usafi na ucheleweshaji tangu kuwavua hadi kuwachakata. Madumu yenye matundu ni aina ya makasha ya gharama nafuu yanayoweza kutumika kuhifadhi na kulinda samaki mara baada ya kuvuliwa na kusafirishwa kutoka kwenye boti hadi katika eneo la uchakataji na kutunza ubora wa samaki hao wabichi.

## Jinsi ya kutengeneza na kutumia madumu yenye matundu


Madumu yenye matundu yanaweza kupatikana kwa urahisi kwa kuyanunua kutoka kwa wasambazaji wa madumu matupu yaliyotumika kuhifadhi bidhaa zisizo za sumu, k.m. mafuta ya kupikia. Chukua kisu cha moto na kata matundu ya ukubwa wa sm1 ya pembetatu upande wa pembeni na chini. Upande wa juu, kata tundu kubwa kwa ajili ya kumiminia na kuwatoa samaki.

Madumu hayo sasa yanaweza kutumika kutunza samaki wakati wavuvi wanapokuwa majini na wakati wa kuwasafirisha hadi ufukweni. Wakati samaki wanapowekwa katika madumu yenye matundu, samaki wanalinda dhidi ya maambukizi na uharibifu huku maji ya ziada yakitoka.

Wakati wavuvi wanapofika ufukweni, madumu yenye matundu yanarahisisha kuwapakua samaki. Samaki hao wanabebwa kwa urahisi kutoka kwenye boti hadi eneo la uchakataji. Kwa kutumia madumu hayohayo kutoka kwenye boti hadi eneo la uchakataji, maambukizo kutoka chombo kingine hadi kingine ambayo yangeweza kutokea maana usafi wa vyombo hivyo vingine haujulikana, yanaepukwa.

## Matunzo sahihi na usafi wa madumu yenye matundu

Baada ya kuwapakua samaki, yaoshe madumu yenye matundu vizuri kwa kuyasugua na kuyasuuza kwa maji safi. Yaweke juani ili yakauke. Usafi mzuri kila baada ya safari ya uvuvi ni muhimu ili kuepuka maambukizo kwa mzigo unaofuatia wa samaki.



Tazama video

[https://youtu.be/q8QoBrP\\_DdM](https://youtu.be/q8QoBrP_DdM)

Pitisha simu kwenye  
alama hii ili kutazama  
video

